

**Dondoo za mukutano wa Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam**  
**Tarehe 27 Octoba 2007**

**Waliohudhuria**

Ally Saidi Mohamedi  
Ally Saidi Mwishehe  
Ally Salum  
Bushira Yahaya Rashidi  
Dominata Rwechungura  
Elaine Baker  
Filbert Mbecha  
Husein Hamza Hamisi  
Juma Ali Salehe Jongo  
Kassim Bakari  
Kibwana Mohammad Msiga  
Paulo Atibu Hatibu  
Rahma Ali  
Sudi Saidi Ramadhan  
Yusufu Juma

**Msafara wa baiskeli**

Wanachama walijadili msafara wa baiskeli wa wiki iliyopita ambaa ulikuwa na mafanikio. Kila mwanachama wa UWABA aliyetakiwa kukamilisha kukumu lake siku hiyo alifanikisha kikamilifu. Juma , Elaine na Mejah walitoa cheki kutoka ubalozi wa uholanzi (Netherland). Juma alinunua majaketi , Mejah alikodisha vifaa vya muziki mahema na aliandaa matangazo kwenye mtanzania na Dar leo na Elaine alinunua helimetni. Dominata aliandaa gazeti la majira ili kuandikwa kwa matukio ya siku hiyo. Juma na Paulo walibaki Mnazi Mmoja usiku kucha kulinda vifaa vya muziki. Jumanne, filbert, yusuf juma na Sudi Saidi chukua maji toka kinondoni na kuyagawa. Allen wa CHABADA alisimamia uelekeo na uslama wa msafara. Juma alisimamia ugawaji wa tiketi za bahati nasibu. Wakati wa msafara wa wakati wa Hotuba, Donata alikuwa mc Mzuri. Sosthenes alirekodi kwa video tukio hili.

Zaidi ya watu 200 walishiriki wakiwemo walemvu, wanaume, wanawake na watoto. Kundi la wanawake liitwalo kali mata toka gezaulole walipanda baiskeli hadi hapa ili kushiriki. Mgeni wetu rasmi alikuwa mshauri wa halmashauri wa wilaya ya ilala akimwakilisha Meya wa Ilala. Allitoa hotuba nzuri akiwaunga mkono wapanda baiskeli. Washindi wa zawadi walifurahi zawadi zao.

Tukio hilo lilioneshwa na channel 10 na ITV taarifa za habari jioni hiyo ikionyesha asahili uliooneshwa na mejah, Elaine Dominata. Hakuna aliyeangalia magazeti ya jumpily au jumatatu kuona kama tukio lilirekodiwa

Wanachama walichukua vibendera vidogo lakini bango kubwa lilionekana. Juma atafuatilia na watu wa mnazi mmoja kama wameliona.

Elaine aliazima UWABA kiasi cha fedha iligharimia kofia (Helmeti) na utoaji nakala, hivyo atarudishwa fedha yake punde tutakapopata fedha toka ubalozi wa Uholanzi.

### **Tukio la kubadilika kwa hali ya Hewa Desemba**

Elaine aliarifu kuwa Desemba kutakuwa na siku ya maandamano dunia nzima kupinga mabadiliko ya hali ya hewa, kikundi cha londoni kiitwacho “campaign against climate change” pamoja na makundi mengine ulimwengu, wanapanga kusimamia tukio hilo siku moja. Ilikubalika kuwa UWABA itashiriki hili kwa kupanda baiskeli hadi ubalozi wa Marekani kuwasilisha barua kuwataka Marekani kusini. Kyoto protocol na kuwajibika kwa kuwa wao ndio wanaochangia kwa kiwango kikubwa uharibifu wa hali ya hewa na viongozi hawazungumzii jambo hili. Ni sahihi kwa UWABA kuwajibika kuonyesha ushirikiano wao kama mfano wa kutoekota kaboni wakati wa usafiri.

Ally saidi Mohammed alipendekeza kuwa tumwombe Bwana Legnard Mengi wa IPP ambaye pia ni menyekiti wa kamati ya mazingira ya serikali ili aunge mkono tukio hili. Bushira alisema kuwa yeche ni ndugu wa direkta wa kamati hiyo. Profesa Jamidu katibu wa chuo kikuu cha Dar es Salaam ili nae ashiriki.

### **Ufuatiliaji wa barua**

Juma alisema atafuatilia majibu ya barua zetu TANROADS na halmashauri ya jiji la Dar Es Salaam

### **Ofisi**

Kwa vile tukio la msafara limekweisha tunaweza kuendelea kuchangia ili kuweka vifaa zaidi kwenye ofisi. Iliombwa kutafuta mtu atakayetafsiri dondo kwa Kiswahili na maelezo ya kwenye internet ili yawekwe kwenye rafu za ofisi. Mtu huyo atalipawa toka kwenye mchango tunaotegemea toka Italia. Ikiwa tayari tutaandaa sherehe ya ufunguzi.

### **Mengineyo**

Elaine alisema hajapata mawasiliano na wamba Memorial Fund ikiwa pendeleko letu limekubaliwa pia mchango toka Italia haujafika kwa sababu ya ugumu wa kuhamisha fedha benki.

Wanachama wawili wageni walikaribishwa na kuomba vitambulisho.